



JARIDA MAAALUM

Toleo la 7 | Agosti, 2020

OFISI YA WAZIRI MKUU



NDANI...

WATANZANIA TUBADILIKE, TUJIVUNIE VYETU

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka Watanzania wabadilike na wajifunze kujivunia kilicho chao.....

TANZANIA NI YA KWANZA AFRIKA KWA KUSAMBAZA UMEME HADI VIJIJINI

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema Tanzania imeshika nafasi ya kwanza barani Afrika kwa kufanikiwa kusambaza umeme nchini kote kwa asilimia 80.....



Ofisi ya Waziri Mkuu



owm_tz



www.pmo.go.tz



JARIDA LA MTANDAONI



WAZIRI MKUU: WATANZANIA TUBADILIKE, TUJIVUNIE VYETU

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka Watanzania wabadilike na wajifunze kujivunia kilicho chao. "Lazima tubadilike Watanzania, tuwe wazalendo, tukisemee kitu chetu, tujivunie kitu chetu na tujivunie ujuzi tulionao," amesema.

Ametoa wito huo Jumanne Agosti 18, 2020 wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa mkoa na wafanyakazi wa kiwanda cha sukari cha Bagamoyo (BSL), katika kata ya Makurunge, wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani.

Waziri Mkuu ambaye alifika kiwandani hapo na kukagua ujenzi wa kiwanda unaoendelea, pia alikagua miundombinu ya mradi wa shamba la miwa ikiwemo vitalu vya mbegu, miche, maabara ya kupima maji na udongo na miundombinu ya umwagiliaji.

"Ninasema tubadilike sababu nimeenda kwenye maabara yao na kukuta wataalamu wetu wako vizuri, wanafanya utafiti wa udongo, maji

na mbegu. Wameelezea vizuri utafiti wao na matokeo tumeyaona ni mazuri."

"Rais wetu alisema Watanzania tunaweza, na leo nimethibitisha kwamba Watanzania tunao uwezo wa kazi lakini tatizo letu hatuwezi kujisemea wenyewe. Lazima tujisifu, tujisemee kuhusu umahiri tulionao. Ni kwa nini tujidharau?", alihoji.

"Nataka tubadilike sababu Watanzania tunaweza. Baadhi yao wanatoka hapa hapa Bagamoyo. Nimemuuliza ulisoma wapi, akajibu Chuo cha Kilimo Kaole, na hiki kiko Bagamoyo. Wengine wanatoka SUA (Chuo cha Kilimo cha Sokoine). Lazima turingie nchi yetu, lazima tuitangaze nchi yetu na ni lazima tuisemee nchi yetu," amesisitiza.

Waziri Mkuu amesema uamuzi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kutoa eneo hilo lenye hekta 10,000 ili lilimwe miwa na kujenga kiwanda cha sukari, ulilenga kuongeza uzalishaji wa sukari nchini. "Tunahitaji kupata mashamba mengi ya miwa ili tuongeze uzalishaji wa sukari nchini.

TANZANIA NI YA KWANZA AFRIKA KWA KUSAMBAZA UMEME HADI VIJIJINI -MAJALIWA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema Tanzania imeshika nafasi ya kwanza barani Afrika kwa kufanikiwa kusambaza umeme nchini kote kwa asilimia 80.

“Leo hii Tanzania ni ya kwanza barani Afrika kwa kusambaza umeme kote nchini hadi vijijini na kufikisha asilimia 80. Kuna nchi ngapi barani Afrika, lakini Tanzania imefanikiwa kuwa ya kwanza. Tumeweza kufikia vijiji 9,112 Tanzania na hadi Aprili 2020 na tumetumia shilingi trilioni 2.27,” amesema.

Ametoa kauli hiyo Jumatatu, Agosti 17, 2020 wakati akielezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye mkutano wa viongozi wa dini kutoka kamati za amani za mikoa mbalimbali Tanzania bara na Zanzibar, uliofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Mwalimu Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na viongozi waliohudhuria mkutano huo uliandaliwa ili kuunga mkono juhudi za Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake katika ustawi wa amani, uzalendo na kumtanzuliza Mungu, Waziri Mkuu amesema ushirikiano mkubwa wanauonesha kwa Serikali, umewezesha kufanya mambo mengi ikiwemo kuimarisha huduma za upatikanaji wa nishati kwa ajili ya ustawi wa Watanzania.

Mbali ya upatikanaji wa umeme nchini, Waziri Mkuu ameelezea mambo mengine 15 yaliyofanyika kwa ufanisi mkubwa chini ya uongozi wa Dkt. Magufuli ikiwemo kurejesha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma; mapambano dhidi ya dawa za kulevya; ulinzi wa rasimali za Taifa; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato na kukua kwa uchumi.

Mengine ni mapambano dhidi ya umaskini na ukosefu wa ajira; ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya afya; maboresho ya elimu; huduma za maji; ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Nyerere, ujenzi wa mradi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR); usafiri wa anga; ujenzi wa meli na bandari na ujenzi wa barabara na madaraja.



KASSIM MAJALIWA
Waziri Mkuu wa Tanzania



WAZIRI MKUU AWEKA JIWE LA MSINGI KIWANDA CHA SAMANI RUANGWA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ametoa rai kwa wawekezaji wachangamkie fursa zilizopo nchini kwa kuangalia maeneo mazuri ya kufanya uwekezaji mpya au kupanua uwekezaji wao.

Ametoa rai hiyo Jumapili, Agosti 16, 2020 wakati akizungumza na wakazi wa Namichiga, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi, waliohudhuria uwekaji wa jiwe la msingi kwenye kiwanda cha samani cha Saw Mill and Furniture Processing Industry na kisha kukagua eneo la ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho wilayani humo.

Waziri Mkuu amesema hicho ni kiwanda cha kwanza kujengwa Ruangwa hivyo amewataka wakazi wa Namkonjera na vijiji vya jirani wapime ardhi yao ili watu wanunue viwanja na kuanza kujenga.

“Kujengwa kwa kiwanda cha kutengeneza samani na baadaye kiwanda cha kubangua korosho, kuta- hamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo na misitu

pamoja na kuimarisha mnyororo wake wa thamani. Endapo mtajipanga vizuri kwa kujenga viwanda vya kuongeza thamani kwenye zao la korosho, wilaya hii itakuwa kinara kwenye uzalishaji wa zao hilo,” amesema.

“Kwa upande wa viwanda, tusiishie tu kwenye korosho, tuone pia namna ya kuwa na viwanda vya kuchakata ufuta, mbaazi na mazao mengine yanalimwa kwa wingi kwenye maeneo yetu ili kijihakikishia soko na upatikanaji wa ajira.”

Amesema uwekezaji huo unaofanyika sasa, unakwenda sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuanzisha na kuendeleza viwanda ili kukuza uchumi, kuleta maendeleo endelevu, kuongeza ajira na kupunguza umaskini kwa Watanzania wote.

Akifafanua kuhusu ujenzi wa viwanda nchini kote, Waziri Mkuu amesema kuimarika kwa uzalishaji hususan kupitia ujenzi wa viwanda, kumekuwa

chachu ya upatikanaji wa huduma hususan kufuatia kuimarika kwa mapato ya Serikali na kutengeneza ajira kwa Watanzania.

Mapema, Naibu Waziri wa Kilimo, Bw. Omar Mgumba alisema uwekaji wa jiwe la msingi Katika kiwanda hicho cha kutengeneza samani, ni matokeo ya msisitizo wa Rais Dkt. John Magufuli na usimamizi wa karibu wa Waziri Mkuu mwenyewe kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Alisema Serikali imepania kuongeza uzalishaji wa zao la korosho ifikapo mwaka 2025. “Wenye viwanda vyote vya korosho, nawahakikishieni kwamba tutakuwa na malighafi za kutosha, tume-panga kuongeza uzalishaji kutokatani 300,000 hadi tani milioni moja ifikapo mwaka 2025,” alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Bw. Hashim Mgandilwa alisema anawashukuru na kuwapongeza Orascom kwa uamuzi wao wa kujenga kiwanda cha samani na cha kubangua korosho kwani utakuwa na manufaa ya kiuchumi na kielimu.

“Ninawakumbusha wawekezaji hawa waweke kipaumbele katika kurudisha sehemu ya mapato yao kwa jamii,” alisisitza.





KUWENI WABUNIFU MUWEZE KUJIAJIRI - MAJALIWA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka vijana wanaohitimu masomo nchini wasikae majumbani na badala yake watumie elimu yao kubuni namna ya kujiajiri.

“Lazima tubadilike ili wahitimu wasisubiri kazi za masomo. Ukimaliza masomo, tumia ujuzi wako kuona unaweza vipi kujiajiri,” alisema.

Ametoa wito huo Jumatatu, Agosti 17, 2020 wakati akizungumza na wahitimu wa Seneti ya Dar es Salaam kwenye mahafali ya vyuo na vyuo vikuu vya jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Karimjee, jijini humo.

“Tunajaribu kuondoa dhana ya ajira ni ile kazi ya kushika kalamu na kukaa ofisini na kulipwa mshahara mwisho wa mwezi. Sasa kama wasomi wote tukitaraji kuajiriwa, hatutaweza. Lazima tukubali kuwa ajira ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu kipato chake,” alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alisema tangu Serikali ya awamu ya tano iingie madarakani imefanya kazi ya kuboresha mazingira ya utoaji wa taaluma kwa kujenga na kukarabati miundombinu katika baadhi ya vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu nchini.

“Ili kuondoa adha ya malazi kwa wanafunzi kwa vyuo na taasisi za elimu ya juu zilizopo Dar es Salaam, Serikali imetoa nyumba za Serikali zilizoko Kigamboni na Kijichi, jijini Dar es Salaam.”

Akizungumzia kuhusu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Waziri Mkuu alisema ujenzi wa maktaba ya kisasa inayochukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja uligharimu sh. bilioni 93. “Ujenzi wa mabweni 20 ya Dkt. John Pombe Magufuli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,840 na ukarabati wa hall 2 na 5, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 788 uligharimu shilingi bilioni 15.48,” alisema.



Kuhusu Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam (DUCE), Waziri Mkuu alisema Serikali ilitumia sh. bilioni 1.5 kujenga miundombinu ya kufundishia na ofisi za wadhiri Katika chou hicho na pia ilitumia sh. bilioni 4.9 kufanya ukarabati mkubwa wa majengo ya Hall 2 na Hall 5 chuoni hapo.

“Kwenye Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) tulitumia shilingi bilioni 11.5 kwa ajili ya ujenzi wa maabara yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja; ujenzi wa Kafeteria ya wanafunzi pamoja na kutengeneza shamba darasa kwa shilingi milioni 700; ukarabati wa karakana ya uhandisi kwa shilingi milioni 750 na ununuzi wa matrekta 10 aina ya URSUS pamoja na majembe nane na harrow mbili kwa thamani ya shilingi milioni 587.5 ili kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa vitendo.”

Akielezea uboreshaji uliofanywa kwenye Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Waziri Mkuu alisema ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 716 uliharimu sh. bilioni 3.44 ilhali Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kilinunuliwa vifaa vya maabara vya thamani ya sh. bilioni 3.0.

“Kwa upande wa Chuo cha Ardhi (ARU), tumeanza na awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 312 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.61,

Na kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), tumejenga jengo la mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa gharama ya shilingi bilioni 8.8. Pia tumejenga maabara kwa gharama ya shilingi bilioni 2.1,” alisema.

Kuhusu Chuo Kikuu cha Mzumbe (MU), Waziri Mkuu alisema ujenzi wa hosteli zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,024 uliharimu sh. bilioni 6.5 huku ujenzi wa jengo la mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 900 ulitumia sh. bilioni 3 katika kampasi ya Mzumbe-Mbeya.

Na kwa upande wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Waziri Mkuu alisema awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuwahudumia wanafunzi 2,500 umekamilika kwa gharama sh. bilioni 5.523.

“Kwenye Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila, ujenzi wa miundombinu ya hosteli zitakazochukua wanafunzi 1,370, ujenzi wa maktaba, kafeteria, madarasa na ukumbi wa mihadhara utagharimu shilingi bilioni 13.3,” alisema Waziri Mkuu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mic Mdegela ambaye ni Mwanachuo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere anayesoma kozi ya Menejimenti ya Rasilimaliwatu baada ya kuzungumza na kutoa vyeti katika Mahafali ya Vyuo na Vyuo Vikuu vya jijini Dar es salaam yaliyo-fanyika kwenye kumbi wa Karimjee jijini Dar es salaam, Agosti 17, 2020

VIONGOZI WA DINI WAMPONGEZA RAIS DKT. MAGUFULI



Katibu wa Kamati ya Amani, Askofu Jackson Sosthenes amesema wameamua kufanya mkutano maalum ikiwa ni lengo la kumpongeza Rais Magufuli kwa hatua iliyofikiwa ambayo Tanzania imefikia uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025.

Ametoa kauli hiyo Jumatatu, Agosti 17, 2020 wakati mkutano wa viongozi wa dini kutoka kamati za amani za mikoa mbalimbali Tanzania bara na Zanzibar, uliofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Mwalimu Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam ambao mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

“Viongozi wa Serikali ya awamu ya tano wameweza kufikia matarajio ya wengi na wamekuwa siyo watu wa maneno mengi. Siri ya yote hayo ni kumtanguliza Mwenyezi Mungu kama ilivyosemwa kwenye maandiko matakatifu kwamba mtafuteni kwanza Mungu na mengine yote mtazidishiwa,” amesema.

Akitoa tamko la viongozi wa dini, Mwenyekiti wa Kamati ya Amani, Sheikh Alhad Mussa alisema ujasiri wa Rais Magufuli wa kutozuia ibada na kukata kufungia watu ndani (lockdown), ulimpendeza Mwenyezi Mungu na akaamua kuifanya Tanzania kuwa nyota inayong'ara ulimwenguni.

Kuhusu uchaguzi mkuu ujao, Sheikh Alhad alisema: “Viongozi wa dini hatuko tayari kushuhudia uvunjifu wa amani ukitendeka nchini. Tunawaomba viongozi wa saisa wahakikishe wanalinda amani yetu na mshikamano wetu.”

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeiry ambaye alikuwa wa kwanza kutoa salamu za viongozi wakuu wa dini, alisema mtu mwenye akili anahitaji pointi ndogo tu kuona kinachofanywa na Rais Magufuli. “Mambo aliyoyafanya Mheshimiwa Rais kwa nchi yetu hayahitaji kufikiri sana kwa sababu yako dhahiri. Amefanya kazi kubwa ndani ya miaka mitano, ambayo yangeweza kufanyika kwa miaka 25.”

Naye Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dkt. Alex Malasusa alisema amani ndiyo msingi wa maendeleo yote. “Amani ni mtaji wa maendeleo. Ukiwa na fedha lakini kama hakuna amani, haziwezi kukusaidia chochote.”

“Viashiria vya ukosefu wa amani hatuvipendi, na tunaviombea vitoweke katika jina la Mungu,” alisema na kuongeza kuwa viongozi wa siasa watambue kuwa yako maisha wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.

“Sisi viongozi wa dini tutaendelea kuiombea nchi yetu. Mungu anaipenda sana Tanzania, na hata tulipopita kwenye bonde la uvuli wa mauti la COVID 19, bado alituvusha. Tuendeleo kumheshimu Mungu, kumtii na tuendeleo kumwabudu Mungu,” alisisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya Mufti wa Zanzibar, Sheikh Nooman Jongo alisema zamani Tanzania iliathiriwa sana na udini, ukabila na uchama lakini kwa sasa hayapo. “Ukiwa Mkristo au Muislamu unapaswa utambue kuwa sisi sote ni ndugu wa baba mmoja, ambaye ni Ibrahimu. Tuangalie amani na upendo na yaliyofanywa na Rais Magufuli hayahitaji tochi ili uyaone,” alisema.

Naye Askofu Michael Hafidhi wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Zanzibar aliwataka viongozi wa vyama vya siasa waache kuwasema wenzao vibaya na kutumia majina ya maaskofu na sheikh kwa manufaa yao binafsi.

“Zamani tulikuwa na siasa chafu, siasa za majitaka. Je sasa hivi zinatoka wapi? Tafadhali tusirudi tena kule nyuma. Wako baadhi ya viongozi wa siasa, wakipanda majukwani wanawasema wenzao, waache mara moja.”

“Tena kuna wanatumia majina ya Masheikh na Maaskofu vibaya. Msitufanyie reference katika majukwaa yenu kwa sababu sisi tunafanyiwa reference na Mwenyezi Mungu. Wakiendeleo kututumia, wajue tunahesabu zao siku,” alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Amani, Mchg. George Fupe alisema wanatoa tamko kwa wagombea wote watakaoenda kujinadi kwenye kampeni ili kutunza amani ya nchi ya Tanzania.

“Tamko letu kwa wagombea wote, lina mambo matatu: Tunawataka wamtangulize Mungu katika utendaji wao, pili watumie busara na hekima wawapo na tatu wazingatie utu wema.”





KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S.L.P 980
40480 Dodoma,
Baruapepe: ps@pmo.go.tz, Simu:+255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz